**INTER ISLAMIC MOCK EXAMIMNATION**

**KISWAHILI 1**

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI**

**2026**

1. Mtahiniwa anapaswa kusoma na kujibu maswali kwa kina kama ifuatavyo:

(a) Kichwa cha habari ni

**MAANDAMANO YA KISIASA/ATHARI ZA MAANDAMANO**

(Au namna nyingine kama inaendana na habari)

- Kichwa kisichopigiwa mstari na kuandikwa kwa herufi kubwa hakitapewa alama.

**(Alama 02)**

(b) Mataifa yaliyoendelea yanatumia propaganda zifuatazo:

(i) Vyombo vya habari **(Alama 01)**

(ii) Kununu wasaliti/vibaraka **(Alama 01)**
(Mtahiniwa anaweza Andika nyinginezo, apewe alama)

(c) Maana ya methali

(i) Mkataa pema pabaya panamwita, ina maana kuwa
Ukikataa neema uliyonayo utaambulia mkosi/balaa. **(01 alama)**

(ii) Vita vya panzi furaha kwa kunguru, ina maana watu wa karibu wanapoingia katika uadui watu wengine hufurahia. **(Alama 01)**

(d) Athari zinazoweza kujitokeza kutokana na janga hilo ni:-

(i) Kuharibika kwa miundombinu **(Alama 01)**

(ii) Kukithiri kwa mauaji **(Alama 01)**

(iii) Kukosekana kwa amani (au nyinginezo)

(e) Namna bora ya kuisaidia serikali ili kuepuka jambo hili ni:

(i) Kutoa elimu **(Alama 01)**

(ii) Kuwajibika **(Alama 01)**

(iii) Kuwa wawazi n.k

Vipengele vitano (05)
Kila kipengele **Alama 02**
**Jumla alama 10**

2. Mtahiniwa aoneshe kwa mifano aina za upatanisho wa kisarufi kama ifuatavyo:

(i) Nomino na kivumishi mfano Mtoto mzuri

(ii) Nomino na kitenzi mfano. Mtoto anakula

(iii) Nomino, kivumishi na kitenzi. Mfano Kijiko kizuri kimepotea

(iv) Kiwakilishi na kivumishi. Mfano Yule mfupi

(v) Kiwakilishi na kitenzi. Mfano Wangapi wanasoma

(vi) Nomino na kishazi tegemezi. Mfano, Mtoto aliyepotea ni wangu

**Hoja 05 @ alama 02 = 10**

(Mtahiniwa atoe hoja na mfano ili apate alama 02)

3. Mtahiniwa afafanue njia zinazotumika kuunda misimu kama ifuatavyo:
(Atoe mfano na maelezo mafupi)
   (i) Njia ya kutohoa. Mfano. Demu – msichana Fegi – Sigara
   (ii) Njia ya ufupisho. Kama kawa, utajiju
   (iii) Njia ya tanakali sauti. Mfano Malapa – Ndala Mataputapu – pombe
   (iv) Njia ya kubadili maana ya msingi ya neno. Mfano kuzimia/kumfia – kupenda sana
   (v) Njia ya sitiari. Mfano Amevaa chupa Amevaa nguo ya kubana

   **Hoja 5 @ alama 02 = 10**

   **(Kila hoja iwe na maelezo mafupi na mfano ilia pate alama 02)**

4. (a) Mtahiniwa atoe ufafanuzi wea kina wa sentensi ambatani na sentensi changamani kwa mfano, kama ifuatavyo:

   Sentensi changamani ni aina ya sentensi inayoundwa na O – rejeshi au viambishi vingine temezi. Mfano. Mbuzi aliyeibiwa amepatikana LAKINI **(Alama 01)**

   Sentensi ambatani ni aina ya sentensi inayoundwa na muunganiko wa sentensi mbili au zaidi. Mfano sentensi sahili na sentensi sahili kwa kutumia kiunganishi mfano. Baba analima na mama anapika **(Alama 01)**

   **(Jumla alama 02)**

   (b) Mtahiniwa abainishe mazingira ya utokeaji wa vielezi na ataje kielezi husika kwa kutoa mfano wa tungo kama ifuatavyo:

   (i) Mazingira ya kuonesha mara ngapi tendo limefanyika au litafanyika.
   - Hapa tunapata kielezi cha idadi. Mfano mtoto amepigwa mara mbili

   (ii) Mazingira ya kuonesha wakati gani tendo linafanyika au litafanyika.
   - Hapa tunapata kielezi cha wakati mfano. Atafika leo asubuhi

   (iii) Mazingira ya kuonesha wapi tendo linafanyika au litafanyika.
   - Hapa tunapata kielezi cha mahali. Mfano. Atakwenda sokoni

   (iv) Mazingira ya kuonesha namna gani tendo linafanyika au litafanyika. Hapa tunapata kielezi cha namna au jinsi. Mfano Anakula polepole

   **(Hoja 04 @ alama 02 = 08 JUMLA ALAMA 10)**

## SEHEMU B ( Alama 60)

5. Mtahiniwa abainishe mambo ya kuzingatia wakati wa uandishi wa Risala kama ifuatavyo:

(i) Kuzingatia lengo la Risala
(ii) Kuzingatia alama za uakifishaji
(iii) Kuzingatia muundo wa Risala
(iv) Kuzingatia mtiririko wa hoja kimantiki katika aya
(v) Kuzingatia matumizi ya lugha fasaha
(vi) Kuzingatia hadhi na mamlaka ya mgeni rasmi na hadhira lengwa.

Hoja 6 @ alama 03 = 18
Utangulizi = alama 01
Hitimisho = alama 01
**(JUMLA ALAMA 20)**

6. Mtahinia aonese mchango wa lugha ya Kiswahili katika sekta ya Elimu kama ifuatavyo:
(i) Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia shule za msingi
(ii) Kiswahili kutumika kama somo shule za sekondari
(iii) Kuchapisha vitabu mbalimbali vya Kiswahili shule ya msingi na sekondari
(iv) Kiswahili kutumika kama somo katika ngazi ya elimu ya juu (vyuo vikuu)
(v) Kiswahili kutumika kama lugha ya kufundishia katika vyuo vya ufundi na vyuo vya kati
(vi) Kiswahili kiliundiwa Baraza lake la kukikuza na kukieneza BAKITA pamoja na asasi nyingine.
(vii) Kutumika kuandaa miongozo ya ufundishaji kwa elimu ya msingi.

Hoja 6 @ **alama 03 = 18**
Utangulizi = **alama 01**
Hitimisho = **alama 01**
**JUMLA ALAMA 20**

7. Mtahiniwa atoe ufafanuzi wa kina juu ya chama cha kukuza na kueneza Kiswahili duniani CHAUKIDU kama ifuatavyo:
(i) Kukuza lugha ya Kiswahili katika Nyanja zote ambazo lugha hii inatumika. Mfano uandishi, habari.
(ii) Kusambaza habari na matokeo ya utafiti kwa kutumia majarida na teknolojia
(iii) Kujumuisha Pamoja wanachama kwa ajili ya kubadilishana Mawazo na ujuzi. Mfano ufundishaji, utafiti, utangazaji nk.
(iv) Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kujivunia na kuheshimu lugha ya Kiswahili.
(v) Kushauri na kushinikiza serikali za nchi wanachama kutambua thamani iliyobebwa na maliasili hii adhimu duniani ili kuunda sera imara ya lugha.
(vi) Kuunga mkono juhudi zinazofanywa na asasi nyingine katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Hoja 6 @ **alama 03 = 18**
Utangulizi = **alama 01**
Hitimisho = **alama 01**
**JUMLA ALAMA 20**

8. Mtahiniwa afafanue kwa kina umuhimu wa udurusu wa Rasimu ya kwanza katika tafsiri kama ifuatavyo:

   (i) Kusahihisha makosa ya kisarufi na miundo isihyoeleweka vizuri

   (ii) Kuonyesha sehemu zenye tafsiri ya mzunguko na zenye matumizi potofu ya visawe

   (iii) Kurekebisha sehemu zenye muunganiko mbaya ambazo zinazuia mtiririko mzuri wa matini

   (iv) Kuhakiki kukubalika kwa lugha iliyotumika katika tafsiri kwa kuzingatia umbo lililotumika kuwasilisha matini lengwa na mada ya matini chanzi.

   (v) Kuona iwapo mada au ujumbe mkuu wa matini chanzi unajitokeza waziwazi katika matini lengwa

   (vi) Kuhakiki usahihi na kukubalika kwa maana zinazowasilishwa katika matini lengwa.

   Hoja 6 @ **alama 03 = 18**

   Utangulizi = **alama 01**

   Hitimisho = **alama 01**

   **JUMLA ALAMA 20**

9.